


KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU



# Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى



Volume 23, Issue 2

18th Rajab 1433

8th JUNE, 2012

## WAJUE VIUMBE VYA ALLAAH "MALAIKA"

NA: SHEIKH MUHAMMAD AL-JIBAALY

**YALIYOMO**

**WAJUE MALAIKA 1 - 4**





## [ENDELEA KUTOKA VOL.23, ISSUE 2]

... kisha mmoja wa Malaika anasema, “lakini miongoni mwao palikuwa na mmoja wao ambaye si katika wao. Yeye alijileta tu kwa ajili ya kitu fulani.” Allaah atasema, “Hata yeye pia nimemsamehe, kwa sababu tu alikuwa amekaa nao. Mtu yoyote atakaeka na watu hao, basi hatokosa kitu.” [al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه)].

**MALAIKA HUONA HAYA.**

Malaika huwaonea haya watu wema. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alieleza hayo kwa Maswahaba wake vipi Malaika walivyokuwa wakimuonea haya ‘Uthmaan Bin ‘Affaan (رضي الله عنه). Alisema (صلى الله عليه وسلم), “Nisimuonee haya mtu huyu, wakati hata Malaika wamuonea haya?”

**HAWAPENDI HARUFU MBAYA**

Malaika hawapendezwi na vitu vibaya visivopendezwa kwa binadamu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) asema: “Mtu anapo kula thaumu, vitunguu, au harufu nyingine mbovu katika vyakula na kurubie msikiti wetu. Hakika Malaika wachukizwa pia na vitu hivyo ambazo wana wa Adam hawavipendi” (Muslim).

**HAWAPENDI MAJIBWA WA MAPICHA –** Malaika hawaigii majumba yenye mbwa au picha na masanamu, kwa sababu Allaah ameviharamisha vitu hivyo. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): “Hakika Malaika hawaingii nyumba zenye mbwa au picha (al-Bukhari na Muslim).

**WANAKWENDA HAJJ –**tumejifunza pia idadi kubwa ya Malaika ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametwambia kuhusu Bayt ul-Ma'moor ni nyumba ilioko mbingu ya saba, mfano wa Ka'bah katika ardhi. Malaika wanaitembelea nyumba hiyo ili wamuabudu Allaah (سبحنه وتعالى). Miongoni mwa wale wanaoingia humo kila siku, alfu sabiini hawatoki tena mpaka siku ya Hukumu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: “Hakika Malaika wapya alfu sabiini wanaingia ndani ya Bayt Ul-Ma'moor kila siku, na hawatoki kutoka humo

**WANA KHOFU KUMUOGOPA MOLA**

**WAO –**Malaika wanamtambua na kumjuwa Allaah (sw) vyema na wanamuogopa kuliko viumbe vyote. Allaah atueleza namna Malaika wanavyo mcha: **[Na vinamsujudi Mwenyezi Mungu vyote venye uhai mbinguni na katika ardhi katika wanyama na Malaika pia nao hawatakabari \*Wanamuogopa Mola wao alie juu yao na wanatenda wanayo amrisha@AN-NAHL 16:49-50]** Hata Jibreel amuogopa Allaah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: “Usiku wa Israa’, nilipita karibu na malaika walioko juu zaidi, Jibreel

alionekana kama zulia lililo fumuka (lililo choka) kwa khofu ya Allaah (سبحنه وتعالى)

**WANASEMA AMEEN KWA DU'AA' –**

Muislamu anapoomba du'aa kumuomba ndugu yake muislamu Malaika anasema “Aameen”. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: “Du'aa ya Muislamu kwa nduguye asiyekuweko yajibiwa na Allaah (سبحنه وتعالى). Kuna Malaika anayebakia naye karibu na kichwa chake nakila akiomba mazuri kwa ndugu yake, Malaika anasema, “Aameen” na kitu mfano wa unayo muomba ndugu yako nawe utapawa” (imepokewa na Muslim kutoka kwa Abu ad-Dardaa (رضي الله عنه)). Na alisema “Wakati imaam akisema “Aameen” na Malaika pia wanasema “Aameen”. Kwahivyo yoyote asemaye “Aameen” wakati mmoja na Malaika madhambi yake yaliopita atasamehewa” (al-Bukhari & Muslim)

**MWISHO –** Imani kwa Malaika yatusaidia kujuwa utukufu wa Allaah (سبحنه وتعالى) katika kuumba kwake katika njia ilio sahihi. Na kwa imani hii vilevile tuelewa kuwa wale wanaomtii Allaah wako wengi zaidi kuliko wanao muasi. Malaika wako wengi sana na vile vile viumbe vyengine vinavyo mtii Allaah (سبحنه وتعالى). Kwa hivyo wanadamu wanao asi wako kidogo ukilinganisha. Na hakika wanamtii ndio Allaah alio radhi nao na atawaingiza katika jannah yake. Imani sahihi kwa Malaika pia yatujaza sisi ni vipi tutastahiki mahaba yaon, na msaada yao na kutuunga kwao.

Haya nikatika mas'ala marefu yanahitaji kusomwa kwa kina zaidi-haya yametolewa katika kitabu cha kiingereza cha Muhammad al-Jibaly (كيتwacho **KNOWING THE ANGELS.**